**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA

**17 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 17 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 175. MHESHIMIWA STANSLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mkoa wa Simiyu ulianzishwa kisheria na Makao yake Makuu kuwa kwenye Mji wa Bariadi badala ya Mji wa Maswa:-

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kuamua Makao Makuu ya Mkoa na shughuli zake yawe Bariadi badala ya Maswa ambako kuna majengo ya Serikali ya kutosha badala yake Serikali inaingia kwenye matumizi makubwa ya kupanga ofisi toka kwa nyumba za watu binafsi huko Bariadi.

(b) Je, Serikali inaweza kufikiria kubadilisha maamuzi hayo kwa manufaa ya Taifa.

**176. MHESHIMIWA SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Jimbo la Kahama Mjini linaathiri sana uzalishaji viwandani hasa ikizingatiwa kuwa Serikali imepiga marufuku baadhi ya viwanda kama vile vya kukoboa mpunga na kusaga mahindi kutofanya kazi usiku:-

Je, Serikali iko tayari kuruhusu viwanda Wilayani Kahama kufanya kazi saa 24 ili kufidia uzalishaji unaokuwa haufanyiki kipindi umeme unapokuwa umekatika hasa nyakati za mchana.

**177. MHESHIMIWA JUMA SELEMAN NKAMIA (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wakulima wengi wa Wilaya ya Chemba wamefukuzwa katika mashamba yao Wilayani Kiteto licha ya kufuata taratibu na kudaiwa kuwa eneo hilo ni hifadhi:-

Je, Serikali ipo tayari kufuta uamuzi uliotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara wa kuwazuia wakulima hawa ili kuondoa mgogoro huo wa muda mrefu.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

### 178. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Mkoa wa Tabora hauna viwanda kabisa na kwa sababu Mkoa huo hulima Tumbaku kwa wingi:-

Je, Serikali inasaidiaje kupata kiwanda cha Tumbaku Mkoani humo.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

### 179. MHESHIMIWA SIXTUS RAPHAEL MAPUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Kumekuwa na ongezeko la Kampuni kubwa kuanzisha mashamba ya Kahawa katika maeneo ya Wilaya ya Mbinga na sehemu za Songwe Vijijini jambo linalotishia uzalishaji na soko kwa wakulima wadogo wadogo wa Kahawa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda wakulima wadogo wasimezwe na wakulima wakubwa.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 180. MHESHIMIWA ZUBER MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wilaya ya Liwale ilipandishwa hadhi kuwa Wilaya kamili tangu Mwaka 1975 lakini ni Wilaya ya pekee ambayo haina kituo cha Polisi wala nyumba za watumishi wa kada hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la kituo cha Polisi Wilayani Liwale sambamba na nyumba za watumishi ambao wanaishi uraiani kwa sasa;

(b) Je, ni lini Tarafa ya Kibutuka itapata kituo kidogo cha Polisi ili kulinda wafanyabiashara wa mazao ya Ufuta wanaokuja Tarafani.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

### 181. MHESHIMIWA PROF. NORMAN ADAMSON SIGALA KING (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Mkoa wa Njombe utaunganishwa na Mkoa wa Mbeya km 205 kutoka Njombe - Makete - Isionje - Mbeya.

**182. MHESHIMIWA SABREENA HAMZA SUNGURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Shirika la Reli Kigoma linawahudumia wakazi kutoka Kigoma, Burundi, Congo, Zambia nk na inawalazimu wakazi hao kulala Stesheni au waamke alfajiri ili kuwahi tiketi na wakati mwingine hukosa tiketi hizo:-

Je, kwa nini Shirika la Reli Tanzania (TRL) wasianzishe mfumo wa uwakala wa tiketi ili kupunguza adha hiyo wanayopata wakazi hao.

**183. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ilani ya CCM iliahidi kutengeneza barabara ya kutoka Njombe - Lupembe - Madeke - Morogoro kwa lami katika Mwaka 2015/2016:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kutengenezwa hasa ikizingatiwa kuwa imebaki miezi 5 katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **17 MEI, 2016** | **KATIBU WA BUNGE** |